

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
TAASISI YA KUZUIA NA KUPAMBANA NA RUSHWA



Barabara ya Kilimatinde
Cheyo,
S.L.P. 1020,
45112 TABORA,
Barua Pepe: rbctabora@pccb.go.tz.
TANZANIA.
www.pccb.go.tz

TAARIFA KWA UMMA

TABORA – Desemba 17, 2020

AFISA MAMLAKA YA VITAMBULISHO VYA TAIFA (NIDA) ADAKWA AKIPOKEA
MLUNGULA

Tarehe 17 Disemba, 2020 TAKUKURU Mkoa wa Tabora inategemea kumfikisha Mahakamani Afisa Mwandikishaji wa Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA) **Bw. JOHN MWENDU JOSEPH** kwa tuhuma za kuomba na kupokea rushwa.

Baada ya TAKUKURU mkoa wa Tabora kupokea taarifa kutoka kwa mwananchi (jina limehifadhiwa) ikimtuhumu **Bw. JOHN MWENDU JOSEPH** kujihusisha na vitendo vya kuomba na kupokea rushwa, ilianzisha uchunguzi ikiwa ni katika kutekeleza majukumu yake kama yalivyotamkwa katika kifungu cha 7 cha Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa Sura ya 329 Marejeo ya mwaka 2019.

Uchunguzi uliofanyika umebaini kuwa, mnamo tarehe 16 Disemba, 2020 katika ofisi za Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa Mkoa wa Tabora, mtuhumiwa aliomba na kupokea hongo ya Shilingi **Elfu arobaini tu (40,000.00)** ili ampatie mwananchi aliyehitaji kupewa huduma ya kupewa namba ya Kitambulisho cha Taifa. Hii ni kinyume na kifungu cha 15(1)(a) na (2) cha Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa Sura ya 329 Marejeo ya mwaka 2019.

Uchunguzi dhidi ya tuhuma hii umekamilika hivyo leo, Mtuhumiwa atafikishwa mbele ya mahakama kujibu mashitaka yanayomkabili.

WITO:

TAKUKURU Mkoa wa Tabora inawakumbusha na kuwataka waatumishi na wakazi wa Tabora kila mmoja kwa nafasi yake kuzingatia sheria, kanuni na taratibu na kujiepusha na vitendo vya

rushwa. Yeyote atakayejihusisha na vitendo vya rushwa atachukuliwa hatua kali kwa mujibu wa sheria.

Tunawashukuru wanahabari, wakazi wa Mkoa wa Tabora na watumishi wa umma wanaoendelea kutupa ushirikiano katika mapambano dhidi ya rushwa. Endeleeni kutimiza wajibu wenu katika vita dhidi ya rushwa nasi tunawaahidi hatutawaangusha.

ASANTENI

Imetolewa na:

MUSA CHAULO

MKUU WA TAKUKURU (M) TABORA